# QUALITY ASSUARANCE SERIRS FORM 1 END TERM 3 EXAMS 2023

## KISWAHILI (QUESTION PAPER)

**FORM ONE**

**TIME 2 HOURS**

**Name**……………………………………………………………………………..
**School**………………………………**Class**…………………………………..
**Signature**…………………………………………………………………
**Date**……………………………………..

**MTIHANI WA PAMOJA WA ZERAKI ACHIEVERS**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| ISIMUJAMII | 10 | |
| FASIHI SIMULIZI | 15 | |
| JUMLA | 80 | |

**1. UFAHAMU**

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Asifuye mvua imemnyea. Hii ni semi yenye hakika isiyopingika, na kuitilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande wa magharibi badala ya mashariki. Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo na kama halipo linakuja. Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini aliushangaza umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina kirefu cha kutamauka na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mafunzo mojawapo ya kidini ambayo padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja yetu ni kushukuru tu. Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

Ima fa ima, na Waswahili husema, Mlaumu nunda na kuku pia." Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kwa kulala nje. Huenda alaikosana na ndugu zake kwa kukwepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia kufidia makosa yake. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na ukimwi , raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa ujumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuwaambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili ni kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto, na hatua inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya P.N. imefafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka. Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la ndoa nje ya ndoa bila haya. Huu upotovu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P.N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu wake.

**MASWALI**

a) Ipe habari hii kichwa mwafaka. (Alama 1)

…………………………………………………………………………………………………

b) Katika aya mbili za mwanzo, mwandishi wa makala haya anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani? (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

c) Eleza chanzo cha tabia za P.N. (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

d) Mwandishi wa makala haya anapendekeza hatua gani ichukuliwe dhidi ya P.N. na kwa nini? (Alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

e) Barua ya P.N. imeonyesha uvumbuzi mpya. Utaje. (Alama 2)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

f) Taja tamathali moja ya lugha iliyotumika katika ufahamu na utoe mfano (alama 2)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumika katika taarifa. (Alama 3)

i) Ima fa ima

………………………………………………………………………………………………

ii) Kufidia makosa yake

………………………………………………………………………………………………

iii) kufanyiana unyama

………………………………………………………………………………………………

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) Kwa kuzingatia hali ya mtetemeko wa nyuzi za sauti, taja aina mbili kuu za sauti. (alama 2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

b) Fafanua muundo wa silabi katika neno Ngwena. (alama 2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

c) Tia shadda katika neno lifuatalo ili kutoa maana mbili tofauti. (alama 2)

Barabara

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

d) Taja vipashio nne vikuu vya lugha. (alama 2)

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

e) Tambua aina zozote tatu za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha kiimbo (alama 3)

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

f) Karabati sentensi hii. (alama 2)

Mgeni ambaye aliyekuja atarudi kesho.

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

g) Kamilisha sentensi zifuatazo ukitumia neno lifaalo kutoka mabanoni (alama 2)

(i) Pahali ........................................ pana mali ................................. (haba, hapa)

(ii) Harun aliiba pesa ............................. akafikishwa .................. (kortini, kotini)

h) Bainisha matumizi ya mshazari katika sentensi ifuatayo

(alama 2) Watoto/wazee walipewa zawadi/tuzo na askofu

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

i) Taja na utoe mifano ya aina mbili za nomino (alama 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

j) Akifisha;

(alama 3)

Mimi nimefurahi sana kuona kwamba umefika mapema je nikuandalie kinywaji gani.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

k) Andika kwa wingi;

(alama 2)

Kondoo huyu na mbuzi yule ni wa mfugaji yupi?

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

l) Kanusha sentensi ifuatayo

(alama 2)

Mimi nilienda dukani

..............................................................................................................................

m) Ni ala zipi za sauti zinazotumika kutamkia sauti zifuatazo? (alama 2)

(i) /b/ ..................................................................................................................

(ii) /th/ ..............................................................................................................

(iii) /v/ ..............................................................................................................

(iv) /g/...................................................................................................................

n) Bainisha maneno yaliyopigwa vistari (alama 2)

Kiatu <u>chake k</u>imeraruka

……………………………………………………………………………………………

<u>Cha </u>kakao kimetafunwa na nguruwe.

..............................................................................................................................

o) Tunga sentensi kulingana na ngeli zilizotajwa. (alama 2)

U – YA.

……………………………………………………………………………………………..

I – ZI

……………………………………………………………………………………………..

p) Geuza sentensi katika kauli ya kutendwa.

Mama anapika chakula kitamu (alama 2)

..............................................................................................................................

.............................................................................................................................................

q) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu (alama 2)

Dada ameenda sokoni

.............................................................................................................................................

r) Tunga sentensi na uonyeshe kundi nomino na kundi tenzi (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

s) Tunga sentensi yenye upatanisho wa kisarufi ukitumia neno **kiroboto** (alama 2)

.............................................................................................................................................

.............................................................................................................................................

**ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana. Kabla ya kujongea mezani pake, Bwana, pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

**Maswali**

a. Tambua muktadha wa dondoo hili (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b. Eleza sifa zozote nne zinazojitokeza katika sajili hii (alama 4)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

c. Umepewa nafasi ya kuzungumza katika mazingira haya. Taja sifa zozote nne za lugha ambazo ungetumia mbali na sifa zilizomo katika dondoo hili. (alama 4)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

**FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)**

**Soma Kifungu kifuatacho kisha ujibu Maswali.**

Ghafla kama ajali, sungura alitokea katika kichaka kilichokuwa karibu, Macho ya mbwa ndiyo yalikuwa ya kwanza kumtua sungura huyo. Moyo wake ukamzaini kukitwaa kisungura hicho na kukonga roho yake. Mara alikumbuka onyo ambalo walikuwa wamepewa na malaika mkuu. Mvutano mkali ulizuka katika nafsi yake, 'Bwana wewe una njaa, vipi utakiacha kitoweo ambacho kwa kweli kinakunyoshea mkono?

i) Hiki ni kipera kipi? Kwan nini? (alama 2)

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………..

ii) Tambua sifa zozote nne za kipera hiki (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

iii) Eleza umuhimu wa kipera hiki. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

iv) Fomyula ya kumalizia hadithi ina umuhimu gani? (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………